# MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA NGARA MJINI



**[*<u>Hili ni eneo la mitambo ya Maji Mukidyama – Ngara Mjini</u>*]**

**<u>RIPOTI YA UTENDAJI YA MAMLAKA YA MAJI ROBO YA I; 2017/2018</u>**

## 1.0 MAJI MJINI

Mamlaka ya Maji Mjini Ngara ilitangazwa kwa **GN Na. 258** tarehe **21 Juni, 2002** na kuanza kazi rasmi tarehe **01 Julai, 2003**. Chini ya sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira **Na.12 ya mwaka 2009** Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Ngara Mjini (NGUWASA), imepewa jukumu la kusimamia na kutoa huduma endelevu ya maji na usafi wa mazingira katika mji wa Ngara chini ya usimamizi wa Bodi ya Maji. Mamlaka iko **kundi C** na **inalelewa na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara**.

## 2.0 UZALISHAJI NA UTOAJI WA HUDUMA YA MAJI

Maji huzalishwa kwa kutumia **mitambo 3** inayotumia nishati ya umeme kutoka kwenye chanzo cha maji cha Mukidyama. Maji husambazwa kwa Wateja kwa njia 2 ambazo ni:-

**(i)**Kusukuma maji hadi kwenye matenki na baadae kuyasambaza kwa mserereko (***Gravity***) hadi kwa wateja na

**(ii)** Kusukuma maji moja kwa moja kutoka kwenye chanzo hadi kwa wateja bila kupitia kwenye matenki (***Direct pumping***)

### 2.1.1 MATENKI YANAYOTUMIKA [UJAZO WAKE JUMLA NI 766$M^3$]

| NA | AINA YA TENKI | UJAZO WAKE | MAHALI LILIPO | ENEO LA HUDUMA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| 01 | TENKI LA MAWE | 250$M^3$ | NYAMIYAGA | Kanda ya Nyamiyaga na Mjini | Linahitaji ukarabati |
| 02 | TENKI LA MAWE | 250$M^3$ | KWA DC | Mjini | Linahitaji ukarabati |
| 03 | FERROCEMENT | 46 $M^3$ | IDARA YA MAJI | Ukanda wa Mzee Sebabili na Ujenzi | Ni zima |
| 04 | TENKI LA MAWE | 75$M^3$ | MUKIDIDILI | Mukididili/Mukirehe | Ni zima |
| 05 | TENKI LA CHUMA | 75$M^3$ | MURGWANZA | Murgwanza/ Mukanywampezi | Linahitaji ukarabati |
| 06 | TENKI LA CHUMA | 70$M^3$ | AFRILINE | Afriline | Ni zima |
| | **JUMLA** | **766 $M^3$** | | | **Ujazo huu ni mdogo** |

### 2.2 IDADI YA WATEJA WENYE MITA [DIRA] ZA MAJI KIKANDA

| Na | JINA LA KANDA YA HUDUMA YA MAJI | IDADI YA MITA [DIRA] ZA MAJI HADI AGOSTI 2017 |
|---|---|---|
| 01 | MUBINYANGE | 640 |
| 02 | NAKATUNGA | 799 |
| 03 | NYAMIYAGA | 728 |
| 04 | MURGWANZA | 403 |
| | **JUMLA** | **2,570** |

### 2.3 AINA YA WATEJA NA IDADI HADI AGOSTI, 2017

| Na | KUNDI | IDADI |
|---|---|---|
| 01 | Watumiaji maji majumbani [Domestic] | 2377 |
| 02 | Taasisi mbali mbali [Institutions] | 113 |
| 03 | Maeneo ya biashara [Commercial] | 47 |
| 04 | Vilula [Viosks] | 33 |
| | **JUMLA** | **2,570** |

### 2.4 HALI YA HUDUMA

NGUWASA ina lengo mahsusi la kutoa huduma ya maji kila siku kwa wakazi wa mji wa Ngara kwa kutumia teknolojia ya mitambo 3 ya kusukuma maji kutoka kwenye chanzo cha maji chini ya ardhi. Katika kipindi cha Julai hadi kufikia Septemba, 2017 hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo mengi ya mji wa Ngara:- Mubinyange, Nyamiaga, Murgwanza, Nakatunga na Buhororo ilikuwa ni ya wastani baada ya kufunga mtambo wa tatu ambao Mhe. Rais alichangia Tsh. 13,000,000 akiwa ziarani Wilayani Ngara. Mtambo ulifungwa kwa jumla

Mh. Rais akiwa ziarani Wilayani Ngara alitoa fedha Tshs. 13,000,000. za kununua mtambo wa 3 na tayari mtambo umenunuliwa na kufungwa kwa jumla ya gharama Tshs. 21,809,180 ambapo gharama nyingine zimetolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara. Mtambo unafanya kazi na umesaidia kupunguza kero ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Ngara.

### 2.5 WATEJA

Katika kipindi kufikia Septemba, 2017 Mamlaka ina jumla ya wateja 2,570

## 2.6 MAPATO NA MATUMIZI

Mapato ya Julai hadi Septemba 2017 ni jumla ya Tsh.49, 182,952 ambapo Tsh. 10,000,000 ni ruzuku kutoka Halmashauri ya Wilaya na Tsh. 39,182,952 ni ya makusanyo ya mauzo ya maji.

Jumla ya Matumizi kwa Mwezi Julai hadi Septemba ni Tsh. 47,416,849. Matumizi makubwa ni ya kununua umeme (LUKU) wa mitambo ya maji Tsh.28, 806,579. Tsh. 18,610,270 imetumika kulipa mishahara, gharama za ukarabati wa miundombinu na uendeshaji ofisi.

## 2.7 MADENI

Hadi kufikia Septemba, 2017, madeni makubwa kutokana na mauzo ya maji yalifikia kiasi cha **Tzs. 30,084,945.00**. Sehemu kubwa ya deni hilo linatokana na baadhi ya taasisi za Serikali: - Magereza **Tzs. 15,790,090,** Polisi **Tzs. 236,320**, Viosks/Vilula **Tzs 1,560,100,** Taasisi nyinginezo (Ngara H/W) **Tzs. 1,869,075.00** na watumiaji wa kawaida wa majumbani **Tzs. 10,629,360**

## 2.8 CHANGAMOTO AMBAZO MAMLAKA IMEKABILIANA NAZO

- Uchakavu wa miundombinu ya maji unaopelekea NRW (upotevu wa maji) kuwa 37.5%
- Ongezeko la madeni ya maji linalosababishwa na baadhi ya wateja binafsi pamoja na taasisi za Serikali kushindwa kulipia maji kwa wakati muafaka.
- Upotevu mkubwa wa maji yanayozalishwa unaosababishwa na mivujo inayotokana na uchakavu wa mfumo wa mabomba uliojengwa zaidi ya miaka 42 iliyopita.
- Kupanda kwa gharama ya umeme wa kuendeshea mitambo ya kusukuma maji na kusababisha Mamlaka ishindwe kutekeleza majukumu yake mengine, kwa mwezi mmoja gharama za ankra za umeme zinafikia wastani wa Tzs. 13,000,000.00
- Mradi kutofanyiwa ukarabati na ujenzi mkubwa kutokana na kutokuwa na fedha za kutosheleza mahitaji halisi.
- Kuchelewa kuanza kwa ukarabati mkubwa wa maji mjini Ngara kupitia “Fedha za World Bank”

## 2.9 MBINU ZA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO ZILIZOPO

- Kufanya matengenezo endelevu ya mara kwa mara ya mfumo wa mabomba ili kudhibiti mivujo
- Kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wateja wanaoshindwa kulipia kwa wakati ankra zao za maji. Pia Barua mbali mbali zimekuwa zikiandikwa kukumbushia ulipaji wa madeni husika kwa Taasisi, Polisi wamepunguza deni lao, Taasisi nyingine bado zinasubiri fedha kutoka Serikalini ili kulipa madeni.
- Mradi kukarabatiwa pamoja na kufanyiwa usanifu na kujengwa upya na hivyo kuondoa mivujo.
- Usanifu wa Mradi wa Maji kupitia World Bank kwa miji 6 [Biharamulo, Kyaka, Chato, Kayanga, Muleba na Ngara] unaendelea na haijajulikana utekelezaji utakuwa lini kwa maana ya kuanza ujenzi. Kati ya tarehe 21 na 23 Machi, 2016 Mhandisi mshauri [*Consultant*] Ms Basler & Hofmann in association with WILALEX & RWB alifika Mjini Ngara kuendelea na usanifu wa kina na mpaka leo hakuna shughuli inayoendelea.

- Makisio ya ujenzi tu wa mradi mzima [bila ya gharama za uendeshaji wake ni jumla ya US Dollar 4,401,989 kufikia mwaka 2025/26 baada ya kukamilika] ni kama ifuatavyo kwa kutumia US dollar:-

| Na | Maelezo/Aina ya kazi | Jumla: *US dollar* | Awamu ya I {2015 - 16} | Awamu ya II {2025 – 26} |
|---|---|---|---|---|
| 01 | P&G (Preliminary and General), Gharama za Jumla | 3,637,521 | 2,084,125 | 1,553,396 |
| 02 | Intake Marine Structure (Ujenzi wa Chanzo darajani Mukajagali) | 68,638 | 68,638 | 0 |
| 03 | Intake Pipe (Mabomba ya kwenye chanzo) | 81,075 | 81,075 | 0 |
| 04 | Transmission Main (Mabomba ya kupandisha maji) | 4,233,000 | 2,116,500 | 2,116,500 |
| 05 | High Lift P.S (Pumping Station) | 985,600 | 492,800 | 492,800 |
| 06 | Water Treatment (Ujenzi wa miundombinu ya kutibu maji) | 2,739,000 | 1,369,500 | 1,369,500 |
| 07 | Storage Tank (Tenki la kupokelea maji) | 780,000 | 390,000 | 390,000 |
| 08 | Electrical (Miundombinu ya umeme) | 642,000 | 642,000 | 0 |
| 09 | Housing (Miundombinu ya majengo) | 600,000 | 600,000 | 0 |
| 10 | Distribution System (Miundombinu ya kusambaza maji) | 21,570,971 | 13,627,822 | 7,943,150 |
| | **JUMLA KUU** | **35,337,805** | **21,472,459** | **13,865,346** |